



Mkulima hodari



Tusome Early Literacy Programme



Mkulima hodari

Tete anaishi katika kijiji cha Panda Mbegu.

Tete ni mkulima aliye na bidii sana.

Anajulikana kijijini kote kwa umaarufu
wake katika ukulima.

Tete hupanda mimea mbalimbali na kufuga
wanyama pia.

Ng'ombe, kondoo na mbuzi hupatikana
katika shamba lake.

Mbali na hayo, Tete hufuga nyuki.





Msimu wa mvua unapofika, Tete
hutayarisha shamba lake.

Kwanza, hukata miti iliyo shambani
akitumia panga na shoka.


Kisha, hufyeka nyasi akitumia fyekeo.

Shamba lake ni kubwa sana na hulilima
kwa kutumia trekta.

Tete hulima shamba lake mara mbili ili
kulainisha mchanga.

Kisha, hutoa mabaki ya nyasi na mimea
akitumia reki.






Baada ya kulima shamba, Tete hutumia
trekta yake kupanda mahindi.

Kazi ya kupanda huchukua siku nzima.
Tete hufurahi sana akimaliza kazi
shambani.

Baada ya kupanda mahindi, Tete huanza kazi katika shamba la mboga.

Shamba la mboga liko kando ya lile la mahindi.

Mboga zake hukua vizuri.





Siku moja Tete alikuta viwavi wamevamia
mboga yake.


Alikasirika kwa sababu ya hasara
aliyopata.

Mazao ya mboga hayakuwa mazuri.

Viwavi ni hatari kwa mimea.

Wao hula majani na kuharibu mimea.

Tete alinunua dawa ya kuwaangamiza.





Tete huzingatia usafi katika boma la wanyama.

Kila wiki, Tete hutia dawa ya wadudu katika zizi la ng'ombe.

Tete hapendi wanyama wake waangamizwe na viroboto.

Tete hupalilia mahindi yake mara mbili na kutia dawa.

Dawa huwaangamiza wadudu na kutoa kwekwe.

Tete amewaaajiri wafanyakazi wawili wanaomsaidia shambani.





Tete hupata mapato mengi kutoka kwenye shamba lake.

Ng'ombe na mbuzi wake hutoa lita nyingi za maziwa.

Yeye huuza maziwa sokoni.



Majirani wa Tete humpenda sana.
Wao huenda kwake kupata ushauri kuhusu
ukulima.
Tete hufurahia kuwaelimisha watu kuhusu
kilimo bora.

Maswali

1. Tete ni maarufu kijijini mwake kwa kazi gani?
2. Tete hufuga wanyama wa aina gani?
3. Tete hutumia vifaa gani kutayarisha shamba lake?
4. Taja aina tatu ya wadudu ambao humsumbuu
Tete katika ukulima wake.
5. Ni mambo gani unayoweza kujifunza kutokana na
ukulima wa Tete?

Mkulima hodari

Tete ni mkulima hodari katika kijiji cha Panda Mbegu. Yeye hutumia vyombo vyakisasa kulimia. Tete huwapatia majirani wake mawaidha ya kilimo bora.



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE



UKaid
from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.